Hotuba ya Kwanza

**KUUTUMIA UJANA VIZURI KUJIJENGA**

**“Umahiri wa Ibada na umahiri wa kazi”**

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa/ Ayman Alasar kitivo cha lugha na ufasiri**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe. Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu:

وَقُلِ اعْمَلُواْ فَسَيَرَى اللّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ.

{**Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye kujua siri na dhahiri, naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wanaomfuata kwa uzuri mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Dini yetu imehusisha uangalifu na umuhimu wakati wa ujana, ikaelezea nafasi yake katika kujijenga, kwani ujana ndio chemchem ya maisha na umri, ni wakati wa kukamilisha ujenzi wa mwili na kukuza akili, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاء وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِير

{**Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na udhaifu kisha akajalia nguvu baada ya unyonge, kisha akajalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba atakavyo. Naye ndiye Mjuzi, Mwenye uweza**}.

Kama vile Sharia ilivyotuongoza kwenye umuhimu wa kutumia vizuri wakati wa ujana katika vile vyenye kunufaisha mwili dini nchi ibada na matendo mema, ambapo Mtume wetu S.A.W anasema:

**اغْتَنِمْ خَمْسًا قَبْلَ خَمْسٍ: شَبَابَكَ قَبْلَ هَرَمِكَ، وَصِحَّتَكَ قَبْلَ سَقَمِكَ، وَغِنَاكَ قَبْلَ فَقْرِكَ، وَفَرَاغَكَ قَبْلَ شُغْلِكَ، وَحَيَاتَكَ قَبْلَ مَوْتِكَ.**

"***Tumia vizuri mambo matano kabla ya matano: Tumia vizuri ujana wako kabla ya kuzeeka kwako, tumia vizuri afya yako kabla ya kuumwa kwako, tumia vyema utajiri wako kabla umasiki wako, tumia vizuri muda wako usio na kazi kabla ya kazi zako na tumia vizuri uhai wako kabla ya kifo chako***". Na anaendelea tena kusema S.A.W:

**لا تَزُولُ قَدمَا عَبْدٍ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حَتَّى يُسْأَلَ عَنْ أَرْبَعِ خِصَالٍ: عَنْ عُمُرِهِ فِيمَا أَفْنَاهُ؟ وَعَنْ شَبَابِهِ فِيمَا أَبْلاهُ؟ وَعَنْ مَالِهِ مِنْ أَيْنَ اكْتَسَبَهُ وَفِيمَا أَنْفَقَهُ؟ وَعَنْ عَلِمهِ مَاذَا عَمِلَ فِيهِ؟.**

"***Hautaondoka mguu wa mja siku ya Kiyama mpaka aulizwe mambo manne: Umri wake ameumaliza vipi, ujana wake ameutumia katika nini, mali zake alizichuma wapi na alizitumia kwenye nini na elimu yake aliifanyia kazi gani***".

Sharia haijatuamrisha kutumia vizuri ujana kwa ibada na kazi tu, bali imetuamrisha pia umahiri na kufanya vizuri kwa sifa ya upekee katika hayo mawili, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **وَأَحْسِنُوا إِنَّ اللهَ يُحِبُّ المُحْسِنِينَ** {**Na fanyeni wema hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao wema**}. Na Mola Anasema tena: **إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ** {**Hakika Mwenyezi Mungu ana amrisha kufanya uadilifu na wema**}. Na Anasema tena: **وَأَحْسِنْ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ** {**Na fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wewe wema**}. Mola akasema tena ndani ya Kitabu chake Kitukufu: **إِنَّ اللهَ لا يَضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا** {**Hakika sisi hatupotezi malipo ya mwenye kufanya wema**}. Na Mtume S.A.W anasema:

**إِنَّ اللهَ يُحِبُّ إِذَا عَمِلَ أَحَدُكُمْ عَمَلًا أَنْ يُتْقِنَهُ.**

“***Hakika Mwenyezi Mungu anapenda mmoja wenu anapofanya kazi afanye kwa umahiri***”.

Umahiri katika ibada unakuwa ni kwa utekelezaji uliosahihi, kukamilisha masharti yake na nguzo zake, kutekeleza sunna zake na adabu zake. Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema kuhusu ibada ya swala: **قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ * الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ**

{**Hakika Waumini wamefaulu * Ambao wanyenyekevu katika swala zao**}. Na Mtume wetu S.A.W anasema:

**أَلا أَدُلُّكُمْ عَلى مَا يمْحُو اللَّهُ بِهِ الخَطَايَا، وَيَرْفَعُ بِهِ الدَّرَجَاتِ؟ قَالُوا: بَلى يَا رسولَ اللَّهِ، قَالَ: إِسْباغُ الْوُضُوءِ عَلى المَكَارِهِ، وَكَثْرَةُ الخطى إِلى المَسَاجِدِ، وَانْتِظَارُ الصَّلاةِ بعْد الصَّلاةِ، فَذلِكُمُ الرِّباطُ، فَذلكُمُ الرِّباطُ.**

“***Je niwafahamisheni jambo ambalo Mwenyezi Mungu kwa jambo hilo hufuta makosa na kuinua daraja? Wakasema: Ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, akasema: Kueneza udhu kwenye viungo, kufanya wingi wa hatua za kwenda Msikitini, kusubiri swala baada ya swala, hayo ndio kizuizi chenu hayo ndio kizuizi chenu***”. Na Mwenyezi Mungu Anasema kuhusu ibada ya zaka:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ أَنفِقُواْ مِن طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُم مِّنَ الأَرْضِ وَلاَ تَيَمَّمُواْ الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنفِقُونَ وَلَسْتُم بِآخِذِيهِ إِلاَّ أَن تُغْمِضُواْ فِيهِ وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ

{**Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa**}.

Kuhusu ibada ya funga Mtume S.A.W anasema:

**إِذَا كَانَ يَوْمُ صَوْمِ أَحَدِكُمْ فَلَا يَرْفُثْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَصْخَبْ، فَإِنْ شَاتَمَهُ أَحَدٌ أَوْ قَاتَلَهُ فَلْيَقُلْ: إِنِّي امْرُؤٌ صَائِمٌ.**

"***Siku mmoja wenu anapofunga basi asitoe maneno machafu wala kugombana, ikiwa atatukanwa na mtu au kupigwa basi na aseme: Mimi ni mwenye kufunga***".

Na anasema Jabir R.A: Pindi unapofunga basi masikio yako yafunge macho yako ya funge na ulimi wako ufunge kwa kutosema maneno ya uwongo na yaliyoharamu, na uwe mpole na mtulivu siku yako ya kufunga, na Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema kuhusu ibada ya hija: **وَأَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ** {**Na timizeni ibada ya Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**}. Na Anasema tena:

**فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَاسِكَكُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا.**

{**Na mkisha timiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyo kuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi**}. Na amri ya kufanya kwa umahiri imejumuisha pia swala la kukafini maiti na kumuandaa, ambapo Mtume wetu S.A.W anasema:

**إِذَا كَفَّنَ أَحَدُكُمْ أَخَاهُ فَلْيُحسنْ كَفَنَهُ.**

"***Pindi mmoja wenu anapomkafini ndugu yake basi na amkafini vizuri***".

****

**Hotuba ya Pili**:

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimuendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa umahiri wa kazi ndio njia ya uma wenye maendeleo, uma ambao unabeba uzalendo kwa nchi yao, na uwelewa wa nafasi yake katika ustawi na maendeleo kwa kufanya kazi vizuri kwa ubora na kwa kipekee, nayo ndio njia bora ya kutumia uwezo wa vijana na nguvu zao katika kuhudumia dini na nchi, kwani sura nyingi za maendeleo ambayo ulimwengu wa leo unayaishi katika Nyanja mbalimbali yamepatikana kwa nguvu ya vijana ambao wamechangia kwa juhudi zao na umahiri wao kumuhudumia mwanadamu.

Sisi tunasisitiza kuwa watu hawataiheshimu dini yetu kama hatutapiga hatua za maendeleo katika dunia yetu, ikiwa tutapiga hatua katika mambo ya dunia yetu watu wataheshimu dini yetu na dunia yetu, na wala hakutakuwa na upigaji wa hatua hizo isipokuwa kwa kufanya umahiri na umakini wa kazi ni utamaduni wa wote kwa kila kitu, katika elimu, uzalishaji wa viwanda, kazi za mikono, bali na pande zote za maisha yetu, tukiwa wenye kufahamu umakini wa kazi ni jambo la lazima wa mafundisho yetu ya Kisharia na ni roho yetu ya kitaifa, kazi hubadilika na kuwa ibada ikiwa itakutanishwa na makusudio matakatifu na malengo makubwa, kwani Mtume S.A.W anasema kuhusu mtu ambaye Maswahaba wa Mtume *Mwenyezi Mungu awe radhi nao* waliposhangazwa na ngozi yake kazi zaka na umahiri wake:

**إِنْ كَانَ يَسْعَى عَلَى وَلَدِهِ صِغَارًا فَهُوَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى أَبَوَيْنِ شَيْخَيْنِ كَبِيرَيْنِ فَفِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى نَفْسِهِ لِيَعِفَّهَا فَفِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى أَهْلِهِ فَفِي سَبِيلِ اللَّهِ.**

"***Ikiwa anafanya kazi kwa ajili ya kuwahudumia watoto wake wadogo basi yupo katika njia ya Mwenyezi Mungu, ikiwa anafanya kazi kwa ajili ya kuwahudumia wazazi wake wawili waliozeeka basi yupo katika njia ya Mwenyezi Mungu, ikiwa anafanya kazi kwa ajili ya nafsi yake ili aitosheleze atakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, ikiwa anafanya kazi kwa ajili ya familia yake pia yupo katika njia ya Mwenyezi Mungu***".

Ewe Mwenyezi Mungu tuwezeshe katika uyapendayo na kuyaridhia…na uhifadhi Misri na watu wake na kila ubaya na chuki.